JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA SABA

06 JUNI, 2016

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA SABA – 06 JUNI, 2016

I. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

303. MHESHIMIWA SILYVESTRY FRANSIS KOKA (KIBAHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Upanuzi wa Hospitali ya Mkoa wa Pwani ijulikanayo kama Hospitali ya Tumbi umesimama kwa takribani miaka mitatu (3) sasa, nondo na zege la msingi na nguzo zinaoza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Hospitali hiyo ili kuondoa hasara na kuleta tija katika huduma ya afya Kibaha.

304. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Dhana ya elimu ni majumuisho ya mambo mengi sana ikiwemo matibabu ya huduma ya kwanza, gharama za umeme, maji, vyakula (kwa shule za bweni), posho za Walimu (*part time*) pamoja na zana za kufundishia zisizohifadhika kwa muda mrefu; na nyingi kati ya gharama hizo zilikuwa zinatatuliwa mashuleni na wakuu wa shule kwa kutumia ada na michango waliyokuwa wanatoza Wanafunzi:-

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha ufanikishwaji wa dhana hii ya elimu bure bila kuanzisha migogoro mipya kati ya Wakuu wa shule, Walimu, Wazazi pamoja na Wanafunzi.

305. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Ujenzi wa Vyumba vya Upasuaji katika Vituo vya Afya vya Bukene na Itobo umekamilika na kwamba vifaa vyote kwa ajili ya kutoa huduma ya upasuaji vimeshafungwa ikiwa ni pamoja na vifaa vya kuhifadhia damu na mashine za kufulia:-

Je, ni jambo gani linazuia huduma za upasuaji kuanza katika vituo hivyo.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

306. MHESHIMIWA KHATIB SAID HAJI (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kutokana na Sheria ya Makosa ya Kimtandao (*Cyber Crime Act*) kuanza kutumika hapa nchini:-

Je, ni mafanikio gani yamepatikana kutokana na kuanza kutumika kwa Sheria hiyo.

307. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya Murushaka ni kiungo muhimu kati ya Karagwe na Kyerwa na ni barabara muhimu sana kiuchumi lakini barabara hiyo ni mbovu sana wala haipitiki kabisa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuitengeneza barabara hiyo ambayo ni muhimu sana kwa Wananchi wa Kyerwa;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga kwa lami barabara hiyo kwa sababu zaidi ya magari asilimia 90 yanayotoka Uganda na Kyerwa hutumia barabara hiyo iliyosahaulika.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:

308. MHESHIMIWA KASUKU SAMSON BILAGO (BUYUNGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi::-

(a) Je, Sera ya Elimu ya mwaka 2014 itaanza kutekelezwa lini katika kipengele cha elimu ya Msingi (Chekechea – Kidato cha Nne);

(b) Je, ni Walimu wangapi wa Sekondari wanahitajika ili kutekeleza Sera hiyo;

(c) Je, hali ya Miundombinu katika shule zetu ikoje katika kutekeleza Sera hiyo.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

309. MHESHIMIWA ABDULAZIZI ABOOD (MOROGORO MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Morogoro Mjini bado ina kero kubwa ya maji katika maeneo mbalimbali ya Manispaa kama vile Kata ya Tungi, Mkundi, Kiegea A na B, Kihonda, Kasanga na Ngerengere:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kero hii ya maji katika Manispaa ya Morogoro.

310. MHESHIMIWA SHABANI OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Jimbo la Lushoto linakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maji hususan katika maeneo ya Ubiri, Makanya, Kwemashai, Gare, Mlola, Mbwei, Malibwi na Kilole:-

Je, ni lini Serikali itawapatia Wananchi hao maji safi na salama ili waondokane na adha hiyo.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

311. MHESHIMIWA DKT. MARY MICHAEL NAGU (HANANG'):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Katika Mwaka wa Fedha 2014/15 Serikali iliunganisha Umeme kwenye Vijiji vinne tu katika Wilaya ya Hanang', hata hivyo Mwaka 2015/16 Serikali iliahidi kuunganisha umeme Vijiji vingine 19:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hiyo ambayo inasubiriwa kwa hamu na Wananchi wa Wilaya ya Hanang'.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

312. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Jeshi la Polisi nchini linafanya kazi kubwa na muhimu ya kulinda usalama wa Raia na mali zao lakini linakabiliwa na upungufu mkubwa wa makazi kwa Askari wake:-

(a) Je, Serikali imepanga kujenga majengo mangapi katika Wilaya mpya ya Itilima na Busega kwa mwaka wa Fedha 2016/17;

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuyakamilisha makazi ya Askari Polisi yaliyopo Wilaya ya Meatu.

II. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Udhibiti wa Matumizi ya Dawa na Mbinu za kuongeza Nguvu Michezoni.

DODOMA
06 JUNI, 2016

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE